

# MPANGO HUU UNATOA HUDUMA KWA NANI?

Watoto na vijana walio na umri wa chini ya miaka 22 ambao hawajahitimu kutoka shule ya upili au hawana cheti sawa na cha shule ya upili wanaweza kustahiki huduma za MEP ikiwa wamehama:

- *nje ya mipaka ya wilaya ya shule; ndani ya miaka mitatu iliyopita; na mzazi/mlezi au peke yao; na*
- *ili kupata ajira ya muda au kwa kilimo cha muda au*
- *ajira ya uvuvi*

Kazi lazima ihusiane moja kwa moja na upanzi, kulima, kuvuna au usindikaji wa mazao; usindikaji wa bidhaa za maziwa, nyama, samaki au samakigamba; au kutunza mifugo. Hakuna mahitaji ya kikabila, asili ya kitaifa, mapato au lugha kwa MEP.



CHANGANUA

## JE, UNAFIKIRI MTOTO WAKO ANASTAHIKI?

Ikiwa unafikiri mtoto wako anaweza kustahiki, tafadhali pigia simu wafanyakazi wa MEP walioorodheshwa kwenye broshua hii. Mfanyakazi wa MEP atakuwa radhi kukutembelea ili kuzungumza kuhusu ikiwa wewe na watoto wako mnaweza kupokea huduma, lakini ni muhimu kwako kupiga simu ili kupata maelezo zaidi. Simu hii inaweza kukusaidia wewe na watoto wako kupata usaidizi wanaohitaji ili kufaulu shuleni. Kuwasiliana na MEP wa eneo lako hakutakusaidia pekee yako tu, kunaweza kusaidia familia nyingine katika jumuiya ya wahamiaji kwa kuleta huduma katika eneo lako. MEP unaweza tu kusaidia watoto wanaostahiki. Tafadhali wasiliana nasi leo.

**WASILIANA NA:**



# Mpango wa Elimu kwa Wahamiaji wa Nebraska

Mpango wa Elimu kwa Wahamiaji wa Nebraska ni mpango unaofadhiliwa na serikali kuu unaoendeshwa na serikali ya jimbo ulioundwa ili kukidhi mahitaji ya kipekee ya watoto wote wa wafanyakazi wa kilimo wanaohama kwa kutoa huduma za masomo ya ziada na usaidizi.



# MPANGO WA ELIMU KWA WAHAMIAJI NI NINI?

Mpango wa Elimu kwa Wahamiaji Kichwa cha I unaofadhiliwa na serikali (MEP) hutoa huduma za masomo ya ziada na usaidizi kwa watoto wahamiaji nchini kote. Mpango huu ulianzishwa mwaka wa 1966 umefanyiwa marekebisha na kuidhinishwa tena mara kadhaa, ikiwa ni pamoja na chini ya Sheria ya Kuhakikisha Kuwa Kila Mwanafunzi Anafaulu ya 2015. Madhumuni ya kijumla ya MEP ni kuhakikisha kwamba watoto na vijana wahamiaji wananufaika kikamilifu kutokana na elimu ya umma bila malipo sawa na inayotolewa kwa watoto wengine. Ili kufikia hili, MEP hutoa msaada kwa mipango ya elimu kwa watoto wahamiaji ili kusaidia kupunguza usumbufu wa kielimu na changamoto nyingine zinazotokana na kuhama mara kwa mara.

# TUNAWEZAJE KUSAIDIA?

Tunajua kwamba ni muhimu sana kwa wazazi kuhusika katika elimu ya watoto wao. Wazazi ndio walimu wa kwanza wa watoto wao. MEP uko tayari kukusaidia katika kumsaidia mtoto wako kujifunza na kukua. Kuhusika kwako kutaonyesha watoto wako jinsi elimu ilivyo muhimu kwa maisha.

# MPANGO HUU UNATOA HUDUMA GANI?

Kila MEP wa eneo hutoa huduma kulingana na mahitaji ya watoto wahamiaji unaowahudumia. Huduma za elimu zinaweza kujumuisha zifuatazo:

- mipango ya kabla ya shule ya chekechea ili kuwaandaa watoto wahamiaji kwa mafanikio shuleni
- mipango ya masomo ya ziada ya majira ya joto
- mipango ya mafunzo maalum
- mipango ya masomo ya ziada nje ya shule
- huduma za usaidizi wa kuhitimu elimu ya sekondari
- Mpango wa Elimu Inayofanikishwa Popote (PASS).
- Mpango wa Kupata Uhitimu Sawa na wa Shule ya Upili (HEP) Mpango wa Usaidizi wa Kifedha kwa Wahamiaji Wanaojiunga na Chuo (CAMP)
- Mwendelezo wa mafundisho kati na miongoni mwa wilaya za shule na fursa za Udhadini wa Masomo za majimbo



[www.nebraska.ne.gov/migrant](http://www.nebraska.ne.gov/migrant)

# HUDUMA / SHUGHULI ZA MSAADA

Zinaweza kujumuisha zifuatazo:

- Baraza la Ushauri la Wazazi (PAC) ambalo huendesha vikao na shughuli nyingine za ushiriki wa wazazi
- uajiri wa watoto wahamiaji jimboni kote
- ushiriki wa maelezo ya wanafunzi kati ya majimbo wakati watoto wanapohama
- huduma za matibabu ya kujumla, ya meno, ya macho na lishe
- huduma za rufaa kwa mashirika mengine ya ndani
- utoaji wa vifaa vya shule

Mipango ya Jimbo ya Elimu kwa Wahamiaji inahitajika ili:

- kuhakikisha kwamba mahitaji maalum ya elimu ya watoto wahamiaji yanatambuliwa na kushughulikiwa;
- kuwapa wanafunzi wahamiaji fursa ya kufikia viwango sawa vya maudhui ya kitaaluma vya jimbo ambavyo watoto wote wanatarajiwa kufikia;
- kukuza uratibu wa huduma za ndani na nje ya jimbo kwa watoto wahamiaji na;
- kuhimiza huduma za elimu ya familia kwa watoto wahamiaji na familia zao.

Matokeo yake ni, watoto wachanga wanatayarishwa vyema zaidi kujiunga na shule, kupata mafanikio ya kitaaluma, kuhitimu, na kujiunga na chuo au kuajiriwa.